
codefa

policy forum




# MWANANCHI

## TUMIA PIMA KADI KUFUATILIA RASILIMALI ZA UMMA

**"Kuanzia kwenye Kijiji au Mtaa hadi kwenye Chanzo Husika"**

**Kimetayarishwa na:**
Community Development for All (CODEFA)

**Kimehaririwa na:**
Kikundi Kai chaTawala Serikali za Mitaa cha Policy Forum
pamoja na Donald Kasongi wa Governance Link

**Kimefadhiliwa na:**
Policy Forum

**Kimesanifiwa na Kupigwa Chapa na:**
Jamana Printers

**Mchora Katuni:**
Simon Regis

**ISBN:** 978-9987-708-41-3

# YALIYOMO

**Dibaji** ..... **ii**

**1.0 UTANGULIZI** ..... **1**

**2.0 IJUE PIMA KADI** ..... **1**

2.1 Jinsi ya Kutumia Pima Kadi ..... **2**

2.2 Hatua Katika Utekelezaji wa Pima Kadi ..... **2**

2.3 Wajibu wa Asasi za Kiraia Katika Uwajibikaji Jamii ..... **3**

2.4 Vigezo vya Uteuzi wa Kamati//Vikundi vya Ufuatiliaji wa Rasilimali za Umma ..... **4**

2.5 Mambo ya Kuzingatiwa na Kijiji/Mtaa katika Kufanya Uteuzi ..... **5**

**3.0 FAIDA ZA KUTUMIA PIMA KADI** ..... **6**

3.1 Huimarisha Juhudi za Serikali ..... **6**

3.2 Huimarisha Uwajibikaji ..... **7**

3.3 Hujenga Mawasiliano Yenye Tija (Constructive Engagement) ..... **7**

**4.0** UFUATILIAJI WA RASILIMALI ZA UMMA KWA KUTUMIA PIMA KADI (SCORECARD) ..... **8**

**5.0 MCHAKATO WA BAJETI NA UWAJIBIKAJI WA JAMII** ..... **13**

**6.0 UHISISHAJI NA UCHECHEMUZI (SENSITIZATION AND ADVOCACY)** ..... **14**

**Rejea** ..... **16**

# DIBAJI

Mwananchi tunayofuraha kukuletea kitabu kiitwacho "Tumia Pima Kadi kufuatilia Rasilimali za Umma" ambacho kitakuwezesha kufuatilia na kulinda rasilimali za umma ili kutimiza wajibu wako wa kikatiba kwa maendeleo ya jamii yetu.

Kitabu hiki ni mkakati wa shirika letu lisilo la kiserikali la Community Development for All (CODEFA) wa kuelimisha na kuwajengea uwezo wananchi ili waweze kuchukua hatua za uwajibikaji kwenye maeneo yao ya Vijiji, Mtaa na Vitongoji ikiwa ni pamoja na kulinda mali za umma, kuzuia uharibifu na ubadhirifu ili waweze kuwa na mwongozo utakaowawezesha kutimiza uwajibikaji wao. Kitabu hiki kitatoa mwongozo wa hatua kwa hatua kwa kuzingatia sheria na taratibu zilizowekwa na serikali.

Wananchi wanahaki ya kufaidi utajiri wa Taifa kwa kupata huduma stahiki ambazo zitaboresha maisha yao sambamba na maendeleo ya nchi, hivyo kila mwananchi anawajibu wa kulinda rasilimali za nchi, kuzitunza vizuri, kupiga vita aina zote za uharibifu na ubadhirifu ili rasilimali hizo ziweze kuendesha uchumi wa nchi kwa manufaa ya Taifa.

Umakini wa mwananchi katika kulinda na kufuatilia rasilimali za nchi ndio njia muafaka ya nchi yetu kupata maendeleo endelevu. Tanzania inaongozwa na serikali yenye kufuata misingi ya demokrasia, hivyo wananchi ndio waamuzi wa hali ya baadaye ya Taifa letu kwa kutimiza wajibu wa kikatiba kwa sababu haki na wajibu ni maendeleo hivyo ni lazima viambatane.

Maudhui ya kitabu hiki yanatokana na katiba ya Jamhuri ya Tanzania 1977, ibara ya 9 kifungu (a) hadi (d) ibara ya 27, ibara ya 29(1), ibara ya 145 na 146.

Tunatarajia kitabu hiki kitachangia kuimarisha uwezo wa jamii katika masuala ya uwajibikaji na ulinzi wa rasilimali za umma, wananchi wataweza kuuliza, kuomba ufafanuzi na kudai uwajibikaji kwa watunga sera na wafanya maamuzi kwa minajili / malengo ya kuwezesha upatikanaji wa huduma stahiki na miundombinu yenye ubora unaolingana na thamani ya fedha husika (Value for money).

Tunatoa shukrani kwa wote waliooneshа juhudi katika kuandaa kitabu hiki kama ifuatavyo., kikundi kazi cha Tawala za Serikali za Mitaa cha Policy Forum (Local Governance Workinng Group) kwa kushiriki kuboresha kitabu, Regina Katabi, Seif Nakuchima, Ruth Bethuel kwa uandishi wa kitabu hiki, Gottfried Mwamanga (CODEFA) na Donald Kasongi (GOVERNANCE LINK) kwa kuhariri andiko hili.

**RUTH BETHUEL**

Kaimu Mkurugenzi - CODEFA

Novemba 2020

# 1.0 UTANGULIZI

Pima Kadi ni mkusanyiko wa viashiria vinavyowekwa na kufuatiliwa na jamii kuhusu usimamizi wa matumizi ya rasilimali za umma. Neno Pima Kadi limetoholewa kutoka kwenye maneno ya lugha ya kiingereza ambayo ni "Score Card" (SC) au Community Report Card (CRC) ikijenga dhana ya kupima na kuonyesha ikiwa wananchi wanaridhika au hawaridhiki na huduma inayotolewa na serikali na wadau/ wawekezaji kwa wananchi.

# 2.0 IJUE PIMA KADI

Pima Kadi (Score card) ni moja ya nyenzo zinazotumika katika kufuatilia uwajibikaji jamii (social accountability monitoring). Pima Kadi hutumika zaidi katika ngazi ya Kijiji na Mtaa kwa sababu ni nyenzo isiyohitaji utaalamu mkubwa. Kwa kutumia Pima Kadi jamii inaweza kufuatilia rasilimali za umma kuanzia kwenye chanzo hadi mtumiaji wa mwisho wa huduma husika.


Sifa kuu ya Pima Kadi ni nyenzo rahisi ambayo wananchi wa kawaida wanaweza kuiandaa na kuitumia kufanya ufuatiliaji wa rasilimali za umma zinazoletwa kuanzia ngazi ya Kijiji/ Mtaa ikiwemo:

(i) Uwepo wa watumishi/ wataalamu kwenye maeneo yao.

(ii) Upatikanaji wa huduma mbalimbali kwenye maeneo yao.

(iii) Miradi ya maendeleo.

(iv) Miundombinu n.k.




## 2.1 Jinsi ya Kutumia Pima Kadi

Wananchi walioteuliwa na vijiji/mitaa wanapaswa kujengewa uwezo ikiwa ni pamoja na kufundishwa hatua za kufuata katika kufuatilia upatikanaji wa rasilimali na kusimamia matumizi ya rasilimali hizo ili kutimiza lengo walilokusudia ambalo ni kulinda rasilimali na fedha za umma. Ufuatiliaji na usimamizi wa rasilimali unalenga kuhakikisha kuwa thamani ya fedha iliyotumika inalingana na miundombinu/miradi husika ama huduma iliyotolewa; wataalam wanakuwepo kwenye vituo vyao vya kazi na kwamba wanatoa huduma ilivyokusudiwa.

## 2.2 Hatua Katika Utekelezaji wa Pima Kadi

Upatikanaji wa taarifa sahihi ni muhimu sana katika kutumia Pima Kadi kufuatilia miradi ya maendeleo na matumizi ya rasilimali za umma. Taarifa husika zinapatikana kwenye Halmashauri husika kwa kufuata utaratibu uliowekwa na mamlaka kwa ajili ya kupata taarifa husika.

(i) Moja ya taratibu za kupata taarifa ni kuandika barua ya maombi kwa mamlaka husika ukiomba kupatiwa taarifa unazohitaji. Baadhi ya taarifa zinazohitaji ni pamoja na Mchanganuo au 'Bills of Quantities (BoQs)' za miradi iliyoidhinishwa na Halmashauri husika inayofuatiliwa

(ii) Mpango wa utekelezaji ukianisha mtiririko wa mahitaji pamoja na fedha zilizoidhinishwa

(iii) Fedha zilizotolewa kwa mradi husika, chanzo cha fedha na hatua iliyofikiwa katika utekelezaji wa mradi.

(iv) Muda wa utekelezaji wa mradi, mkandarasi n.k

(v) Miradi iliyoibuliwa na wananchi wa Vijiji/Mitaa husika kupitia mfumo wa fursa na vikwazo kwa maendeleo ulioboreshwa (O & OD).

Baada ya ufuatiliaji wananchi wanapaswa kuwasilisha matokeo ya ufuatiliaji husika kwa watunga sera na wafanya maamuzi ili waweze kuchukua hatua stahiki kwa ajili ya kuboresha huduma mbalimbali za kijamii kwa ustawi wa wananchi na maendeleo endelevu.

## 2.3 Wajibu wa Asasi za Kiraia katika Uwajibikaji Jamii

Asasi za kiraia zinazofanya shughuli za uwajibikaji jamii (Social Accountability) zinapaswa kusaidiana na wananchi ama kamati za ufuatiliaji kwenye vijiji/mitaa katika maeneo yafuatayo:

(i) Kuainisha taarifa zinazohitajika katika kufanya Pima Kadi na kuziomba kwa mamlaka husika.

(ii) Kujengea uwezo kamati, vikundi au wananchi walioteuliwa na Vijiji/ Mitaa kwa ajili ya kufuatilia rasilimali za umma kwenye vijiji/mitaa yao.

(iii) Kufuatilia zoezi la ukusanyaji wa taarifa.

(iv) Kuchambua taarifa zilizokusanywa na kuandaa taarifa ya awali kulingana na Pima Kadi

(v) Kushiriki kwenye mikutano ya mrejesho na maazimio kwenye ngazi mbalimbali.

(vi) Kushirikiana na wadau wengine kufuatilia utekelezaji wa maazimio yaliyofikiwa kwenye mkutano wa mwisho na kufanya mrejesho kwa wananchi (vijiji na mitaa husika).

Ni lazima vigezo vya kuingia kwenye kamati/vikundi vya ufuatiliaji wa rasilimali za umma

vibainishwe na kuzingatiwa wakati wa kufanya uchaguzi/uteuzi kwenye vijiji/mitaa.

Wajumbe kwa kila Kijiji/Mtaa ni kati ya watu watano (5) hadi tisa (9) kulingana na wingi wa vitongoji na ukubwa wa eneo pamoja na idadi ya wakazi.

## 2.4 Vigezo vya Uteuzi wa Kamati/Vikundi vya Ufuatiliaji wa Rasilimali za Umma



Anayechaguliwa kuwa mjumbe wa Kamati/Kikundi cha ufuatiliaji wa rasilimali za umma ni budi:

(i) Awe mkazi wa kudumu wa Kijiji/Mtaa husika

(ii) Ajue kusoma, kuandika na kuhesabu kwa ufasaha

(iii) Awe na afya njema

(iv) Awe na umri kuanzia miaka 18 na kuendelea

(v) Awe na moyo wa kujituma na kujitolea

(vi) Awe mwaminifu, mwadilifu na mchapakazi

(vii) Awe anajiamini

(viii) Anayekubalika na jamii katika Kijiji/Mtaa wake

(ix) Awe mbunifu, msikivu na anayependa ama kukubali kujifunza

(x) Awe raia wa Tanzania

## 2.5 Mambo ya Kuzingatiwa na Kijiji/Mtaa katika Kufanya Uteuzi

Katika kuteua Kamati ya ufuatiliaji Kijiji/Mtaa ni lazima kuzingatia yafuatayo:

(i) Kuzingatia usawa wa kijinsia. Mfano Mwanaume/ Mwanamke na wenyeulemavu.

(ii) Angalizo: Mwenyeulemavu, Mwanaume au mwanamke ni lazima awe na vigezo vilivyobainishwa katika sehemu ya 3.2 hapo juu.

(iii) Uteuzi uzingatie uwakilishi kutoka kwenye vitongoji vyote vya Kijiji au maeneo yote yamitaa

(iv) Wajumbe wasipungue watu watano (5) na wasizidi tisa (9)

(v) Hata hivyo idadi ya wajumbe inayohitajika inategemea wingi wa vitongoji ama mitaa. Mwakilishi mmoja anapaswa kutoka katika kila kitongoji au mitaa ya kawaida. Wataaalamu (wawezeshaji) wataweza kuelekeza kulingana na jiografia ya Kijiji/Mtaa husika au idadi ya wakazi.

# 3.0 FAIDA ZA KUTUMIA PIMA KADI

Matumizi ya Pima Kadi yanaleta faida kuu tatu kama ifuatavyo:

## 3.1 Huimarisha Juhudi za Serikali

Taarifa zinazotokana na wananchi kufuatilia utekelezaji wa miradi na usimamizi wa raslimali za umma kwa kutumia Pima Kadi huchangia kuimarisha juhudi na mikakati mbalimbali ya serikali ya kuondoa umaskini wa kipato na usio wa kipato kwa wananchi wake, hasa walio pembezoni na wasioweza kusikika kwa urahisi kutokana na vikwazo mbalimbali. Taarifa hizo husaidia kuchambua matokeo ya muda mfupi na mrefu kutegemea aina ya miradi ambayo serikali imetekeleza.

Kwa kutumia Pima Kadi wanajamii huweza kuibua kiuvumbuzi mafanikio na kuonyesha mapungufu yaliyopo ama yanayojitokeza kwa kuhusisha rasilimali zinazoletwa kwenye jamii. Wanajamii huweza kubaini rasilimali zilizotolewa kwa ajili ya kuhudumia jamii au ujenzi wa miundombinu na baada ya hapo kuanisha matokeo ya matumizi ya rasilimali hizo kwenye miradi husika na huduma nyingine zilizotolewa na serikali kwa ajili ya maendeleo endelevu na matokeo ya muda mrefu.

Aidha, taarifa za ufuatiliaji kwa kutumia Pima Kadi huwezesha wananchi kuongea ama kupaza sauti kwa njia ya takwimu, maandishi na mikutano ya hadhara/kisheria kwa kuelezea jambo husika kwa undani, bayana, umakini na kutaka ufumbuzi upatikane kwa mambo ambayo wanayatilia shaka ama hawaridhiki na wanahitaji kujiridhisha kwa njia ya uwazi/rasmi.

Kwa upande wa jamii, ufuatiliaji kwa kutumia Pima Kadi huwajengea uwezo wa kuanisha taarifa wanazohitaji, kuzitafuta, kuchambua na kuelewa kwa undani ujumbe wa taarifa hizo. Uelewa huu husaidia katika kujenga hoja kwa mambo wanayobaini na kuwapa ujasiri wa kuweza kupeleka hoja hizo kwenye mamlaka za juu za serikali na nguvu ya kuzitetea hoja hizo.

Pima Kadi ni nyenzo inayofaa kutumiwa mara kwa mara na wanajamii kwa ajili ya kuleta udhibiti na usimamizi thabiti wa rasilimali za umma kwa kusimamia, kufuatilia na kuangalia mwenendo wa viashiria mbalimbali. Pima Kadi inaweza kutumika kwa njia tofauti kulingana na matakwa au mahitaji ya jamii husika ikiwemo kutathimini miradi iliyokwishafanyika kwa maana ya miradi iliyokamilika, miradi isiyotumika ama ambayo haikukamilika, uwepo wa huduma na ufanisi wa huduma husika/zitolewazo.


## 3.2 Huimarisha Uwajibikaji

Matumizi mazuri ya Pima Kadi yanasaidia jamii kufuatilia jinsi rasilimali za umma, ikiwa ni pamoja na fedha za bajeti ya serikali zilivyotumika, na kubaini kama matumizi ya rasilimali hizo yanaleta matokeo hasi au chanya. Aidha. kwa kutumia Pima Kadi wanajamii wanaweza kutoa taarifa zinazo onesha namna Serikali za Mitaa pamoja na taasisi mbali mbali za umma zinavyojishughulisha na vipaumbele vya jamii na kiwango ambacho jamii huridhishwa na utendaji wa taasisi hizo. Pia taarifa hizo huweza kuibua gharama zilizofichika katika matumizi ya rasilimali na kufichua mianya ya matumizi mabaya ya rasilimali ikiwemo rushwa.Taarifa za aina hii huchochea uwajibika wa watendaji katika taasisi zote zinazohudumia jamii.

## 3.3 Hujenga Mawasiliano Yenye Tija

Msingi mkuu katika ufuatiliaji wa kutumia Pima Kadi ni upatikanaji wa taarifa sahihi na za kuaminika kutoka kwenye vyanzo visivyotiliwa shaka. Hivyo hapana budi kuwepo utashi wa dhati, uwazi na ushirikiano kutoka kwa viongozi wa kisiasa (Wenyeviti wa Vijiji/Mitaa, Madiwani na Wabunge) na Watendaji Wakuu wenye kufanya maamuzi serikalini ili kuwezesha taarifa zinazohitajika katika kufanikisha zoezi la Pima Kadi zinapatikana kwa wakati. Hii ni pamoja na wananchi/jamii kupatiwa kwa wakati mrejesho wa taarifa/maazimio waliyoyawasilisha ngazi za juu kwa ajili ya kupatiwa ufafanuzi/ufumbuzi na majibu sahihi yenye majawabu ya kumaliza tatizo linalowakosesha haki ya kufaidi/kunufaika na


huduma zitokanazo na rasilimali za umma kwa ustawi wao na vizazi vijavyo.Katika kufanya hivyo jamii hujenga mawasiliano yenye tija na serikali pamoja na taasisi zinazohudumia jamii.




## 4.0 UFUATILIAJI WA RASILIMALI ZA UMMA KWA KUTUMIA PIMA KADI

Ufuatiliaji kwa kutumia Pima Kadi hufuata hatua 7 hadi 17 mpaka kukamilika. Hatua hizo zinatofautiana kulingana na suala linalofuatiliwa, na kiwango cha ufuatiliaji. Unaweza kupunguza ama kuongeza hatua kulingana na mahitaji ya wakati lakini ni lazima uzingatie madhumuni ya kufanya ufuatiliaji, sheria na taratibu zinazokuongoza ili ufuatiliaji huo uweze kutimiza lengo na kuleta tija kwa Taifa.

Ili kufanikisha ufuatiliaji wa rasilimali za umma kwa kutumia Pima Kadi ni muhimu kufuata hatua zifuatazo:




1. Kuomba idhini ya kufanya ufuatiliaji na kupatiwa nyaraka zinazohitajika kwa mamlaka husika.
2. Kutoa taarifa kwa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya/Mji/Manispaa/Jiji Watendaji wa Vijiji/Mitaa na Katibu Tawala - Ofisi ya Mkuu wa Wilaya..
3. Kutambua washiriki wa warsha, kupanga mikakati ya kufanikisha ufuatiliaji kwa kutukia Pima Kadi na kufanya warsha. Baadhi ya washiriki wa warsha ni pamoja na;
   - (i) Vyombo vya uangalizi ngazi ya Wilaya
   - (ii) Kitengo cha ukaguzi wa ndani cha Halmashauri
   - (iii) Wawakilishi wa idara, wakala au vitengo vitakavyofikiwa na Pima Kadi
   - (iv) Kamati ya mipango, fedha na uchumi ya Halmashauri - madiwani
   - (v) Afisa maendeleo ya jamii wa wilaya
   - (vi) Wawakilishi wa wananchi – eneo la ufuatiliaji

(vii) Afisa Tarafa wa eneo la ufuatiliaji.

4. Pima Kadi ijadiliwe kabla ya kuitumia, endapo kuna maboresho ya msingi yaingizwe kwenye Pima Kadi. Baada ya maboresho kufanyika, Pima Kadi itakuwa imekamilika kwa ajili ya matumizi ya ufuatiliaji wa matumizi ya umma kwenye eneo husika.

5. Kufanya mikutano ya hadhara kwenye vijiji/mitaa husika kwa ajili ya:

   (i) Kutoa elimu na ufafanuzi kuhusu rasilimali za umma na umuhimu wa wananchi kufanya ufuatiliaji.

   (ii) Kutambulisha Pima Kadi

   (iii) Kuteuliwa kwa wanavijiji/wanamtaa ili kuunda kamati/vikundi vya ufuatiliaji (kama havipo) kwa kuzingatia vigezo na vitongoji wanamoishi.

6. Kuzipatia mafunzo ya kujenga uwezo kamati/vikundi vya ufuatiliaji ya;

   (i) Nadharia: Ikihusisha Pima Kadi, sheria, bajeti, O&OD, uhakiki jamii.

   (ii) Vitendo: kufanya ufuatiliaji wa majaribio kwenye jamii na miradi.

   (iii) Kujifunza kuchambua taarifa walizokusanya, kuandika taarifa na namna ya kukabiliana na changamoto walizokutana nazo kwenye jaribio.

7. Kamati kuanza rasmi kukusanya taarifa kwa wananchi kwenye vijiji/mitaa na miradi husika kwa kutumia Pima Kadi.

8. Kufanya uhakiki jamii endapo taarifa zilizokusanywa zinahusisha miundombinu kama vile Mashamba, Ardhi, Madaraja, Visima vya Maji, Josho, Barabara, majengo ya aina mbalimbali n.k.

9. Wataalamu (wawezeshaji) kusimamia na kufanya ufuatiliaji wa ukusanyaji wa taarifa za Pima Kadi.

10. Wataalam (wawezeshaji) kusaidia kuchambua taarifa zilizokusanywa na kamati/vikundi vya ufuatiliaji.
11. Wataalam (wawezeshaji) kusaidia kuandika taarifa ya awali
12. Taarifa ya awali kurejeshwa kwenye Kijiji/Mtaa
13. Kuitishwa kwa mkutano wa hadhara wa Kijiji/Mtaa kwa ajili ya wananchi kupatiwa mrejesho wa kazi iliyofanyika ili waweze kufahamu kulichomo ndani ya taarifa
    - (i) Waweze kujadili kwa pamoja, wafanye masahihisho pale inapobidi.
    - (ii) Wapitishe taarifa husika ili iwe taarifa rasmi ya wanakijiji/wakazi husika kwa ajili ya kupatiwa majibu na/ama ufafanuzi toka Halmashauri husika.
14. Halmashauri ya Wilaya/Manispaa kupelekewa taarifa zenye hoja za wananchi ili ziweze kupatiwa majibu sahihi na kwa wakati.
15. Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri/Manispaa kutoa majibu/ufafaunuzi kwa maandishi kulingana na hoja zilizowasilishwa kwake.
16. Waatalam/wawezeshaji pamoja na kamati/vikundi vya ufuatiliaji wa rasilimali za umma,watapitia majibu ya maandishi waliyopokea kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri/Manispaa na kuyalinganisha na hoja za wananchi zilizowasilishwa kwake kwa maandishi pamoja na hali halisi ilivyo kwenye Kijiji/Mtaa au miradi husika na kuamua kama ifuatavyo:
    - (i) Endapo majibu waliyopatiwa yamekidhi ama yamejibu hoja zao na kuwawezesha kusonga mbele na/ama kupata wanachohitaji, kitakachofuata ni kufanya mrejesho kwa wakazi/wanakijiji husika pamoja na wadau waliotajwa kwenye hatua ya 3 ya Pima Kadi (washiriki wa warsha)

(ii) Endapo watabaini majibu waliyopatiwa hayakukidhi/hayakujibu hoja zao, basi watayaainisha mapungufu waliyobaini kwa kunukuu hoja husika na kuwasilisha kwa maandishi kwa Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri husika na kumjulisha tarehe ambayo mkutano wa wadau (wa mwisho) utafanyika, ambapo Mkurugenzi na/ama wataalamu wake watautumia kutoa maelezo ya ufafanuzi uhalalisho wa jambo/hoja husika.

17. Kufanyika kwa mkutano ngazi ya Wilaya kati ya Wananchi, Kamati za Ufuatiliaji, Wadau, Wawezeshaji, Wataalamu/ Viongozi wa Halmashauri ya Wilaya/Manispaa ili:

(i) Kupata ufafanuzi na uhalalisho wa majibu ya Mkurugenzi wa Wilaya/Manispaa kulingana na Taarifa za Pima Kadi na hali halisi ya miradi iliyofuatiliwa.

(ii) Kuweka maazimio ya pamoja na hatua mbalimbali za kufanya/kuchukuliwa

(iii) Maazimio kukabidhiwa kwa vyombo vya usimamizi, asasi za kiraia na wadau wengine kwa ajili ya kufuatilia hatua zilizochukuliwa kuhusiana na maazimio husika na kuvijulisha vijiji/mitaa husika kadri ya mgawanyo wa majukumu kisheria ama watakavyojipangia.

Wadau wafuatao watahusika kufuatilia maazimio na kufanya mrejesho;

(a) Kitengo cha ukaguzi wa ndani cha halmashauri

(b) Mkaguzi wa ndani wa Halmashauri husika,

(c) Vyombo vya uangalizi ngazi ya Wilaya.

(d) Baraza la Madiwani-kamati husika kwenye Halmashauri/ Manispaa husika

(e) Mashirika 2 yasiyo ya kiserikali ngazi ya Mkoa/Taifa.


# 5.0 MCHAKATO WA BAJETI NA UWAJIBIKAJI WA JAMII

Ili lengo la kukuza ushiriki wa jamii katika ulinzi wa rasilimali za umma ni muhimu kupanua uelewa wao wa mchakatto wa bajeti na uwajibikaji jamii. Maswali ya msingi kwa mwananchi ili kumuwezesha kuelewa vema mchakato huo ni pamoja na kuelimisha kuhusu:

1. Bajeti ni nini?
2. Sera ni nini?
3. Uwajibikaji jamii ni nini?
4. Fursa na vikwazo kwa maendeleo (O& OD) ni nini?
5. Madaraka ya umma maana yake ni nini?
6. Kwa nini tuwe na bajeti?
7. Bajeti ni sera ama sheria?
8. Nani wanahusika kwenye mchakato wa bajeti?
9. Hatua za mchakato wa bajeti ni zipi?
10. Sera ya bajeti ni kitu gani?
11. Mipango shirikishi jamii inahusiana vipi na bajeti?
12. Bajeti kwa mtazamo wa kijinsia maana yake nini?
13. Kwa nini usimamizi na udhibiti ni muhimu?
14. Kwanini uwazi na uwajibikaji katika bajeti ni muhimu?
15. Kwa nini wananchi wanapaswa kushiriki kwenye mchakato wa bajeti na uwajibikaji jamii?
16. Haki za kijamii maana yake nini?
17. Ugatuzi wa madaraka (D by D) ni nini?
18. Haki na wajibu muhimu maana yake nini?

# 6.0 UHISISHAJI NA UCHECHEMUZI

Wakati wa kufanya ufuatiliaji kwa kutumia Pima Kadi ni muhimu pia kutoa uhisishaji na uchechemuzi (sensitization and advocacy) kwa lengo la kupanua uelelwa wao kuhusu rasilimali na kutia hamasa dhamiri ya mwananchi ili ajiamini kwamba yeye ni mlinzi wa rasilimali za umma na atimize wajibu wake.



Mwananchi tambua kwamba rasilimali za umma ni pamoja na:

| | |
|---|---|
| **Fedha** | Mapato na matumizi. |
| **Vitu** | Majengo, mitambo na miundombinu ya umma. |
| **Watu** | Raia, jamii/wananchi. |
| **Watumishi** | Waajiriwa kwenye shughuli za umma kuanzia Mtendaji wa Kijiji/Mtaa hadi Rais wa nchi. |
| **Mali asili** | Uoto, misitu, wanyamapori, wadudu, n.k. |
| **Mali asilia** | Madini, mafuta, gesi n.k. |
| **Ardhi** | Milima, mabonde, mbuga, bahari, ziwa.n.k. |

Mwananchi fahamu kuwa:

1. Ni haki yako kushiriki na kushirikishwa kikamilifu katika michakato yote inayohusu maendeleo kwenye Mtaa/ Kijiji chako.
2. Ni muhimu kuzifahamu sera mbalimbali za nchi ili ziweze kukuongoza katika michakato mbalimbali.
3. Ni wajibu wako kulinda rasilimali za umma.
4. Rasilimali za umma ni kwa manufaa ya Taifa na vizazi vijavyo.
5. Zingatia kufuata sheria na taratibu zilizowekwa katika kufuatilia rasilimali za umma na huduma zinazotolewa ama kuletwa kwenye kijiji au mtaa wenu.
6. Ni haki yako kupata huduma bora za kijamii.
7. Uwajibikaji, Uadilifu na Uwazi ni nguzo muhimu katika ulinzi wa rasilimali za umma.
8. Timiza wajibu wako wa kikatiba
9. Haki za kijamii ni muhimu kwa ustawi wa binadamu.

10. Ni haki yako kuzifahamu rasilimali mbalimbali zinazoletwa kwenye Mtaa/Kijiji chako na kufuatilia huduma zinazotolewa kwenye Jamii, Kijiji ama Mtaa wenu.
11. Haki na wajibu huambatana, havipaswi kutenganishwa.
12. Unawajibu wa kuhudhuria mikutano ya kisheria ya Mtaa wako au Kijiji chako ili uweze kushiriki kwa namna mbalimbali ikiwemo kupaza sauti kwa ajili ya kuleta tija/ ufanisi ama kudai maboresho kwa ajili ya ustawi wenu na maendeleo ya nchi.
13. Ni lazima utambue kwamba watu (Binadamu ni moja ya rasilimali za msingi katika kuleta maendeleo. Watu hao wanapatikana kwenye Vijiji na Mitaa, wewe ni mmoja wa watu hao, tumia fursa uliyopewa kikatiba na kisheria kujiletea maendeleo.
14. Paza sauti ili wafanya maamuzi na watunga sera wakusikie na wafanye maamuzi sahihi na watunge sera zenye tija kwa mwananchi mmoja mmoja, na maendeleo endelevu ya Taifa.

# REJEA

1. CODEFA Score Cards No. 1,2,3,4; 2009
2. Dira ya Taifa ya Maendeleo, 2025 (Ofisi ya Rais - Tume ya Mipango) Dar es salaam, 2002
3. Fuatilia pesa, Mwongozo wa kufundisha namna ya kufanya PETs ulioandaliwa na Hakikazi catalyst, REPOA na TGNP na kuchapishwa na Policy forum – Dar es salaam
4. Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, 1977.
5. Sera ya maendeleo vijijini, Decemba 2003 (Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania)
6. Social accountability Guide, created by MUHURI – Mombasa Kenya.
7. Taarifa za ufuatiliaji Rasilimali kwa kutumia Pima Kadi uliofanywa na CODEFA 2011 – Kisarawe District Council Nyanja za kilimo, mifugo na miundombinu
8. Taarifa za wananchi na uhakiki jamii volume 1 & 2 majengo ya shule, nyumba za walimu, visima vya maji na zahanati - Mzenga Kisarawe District
9. The social Accountability Monitoring System Guide - PSAM ( South Africa)
10. Ufuatiliaji wa huduma na uwajibikaji jamii ngazi ya mtaa/ kijiji - Mkoa wa Dar es salaam & Pwani: score cards No: 017 - A, B&C
11. Ufahamu Mchakato wa Bajeti: July 2008; Policy Forum & HakiElimu

policy forum

S.L.P. 38486
Dar es Salaam, Tanzania
Simu +255 22 2780200,
+255 782317434
Tovuti: www.policyforum.or.tz
Baruapepe:info@policyforum.or.tz

CODEFA

Community Development for All - CODEFA
Sanze Road 378/E.
Ofisi za miradi: MZENGA & NGORONGO
S.L.P 28029 Kisarawe,
COAST REGION – Tanzania (EA)
Email: ccodefa2@yahoo.com
Web: www.codefa.or.tz